# FAHAMU HAKI ZAKO WAKATI WA JANGA KUBWA LA VIRUSI VYA KORONA

Welcome the stranger. Protect the refugee.

*Kuenea kwa Virusi vya korona au COVID-19 kumebadilisha maisha ya kila siku ya mamilioni ya watu kote nchini Marekani. Mwongozo huu ulioundwa na HIAS, unatoa taarifa kwa wakimbizi, waliokimbilia usalama, waliomo maeneo ya kujisalimisha na wahamiaji wengine kuhusu haki walizo nazo wakati huu wa kipekee. Iwapo una maswali yoyote kuhusu maudhui ya mwongozo huu au iwapo unatafuta rasilimali katika eneo lako, tafadhali wasiliana na msimamizi wa kesi yako au shirika la msaada katika eneo ulipo. Unaweza pia kukagua viungo vilivyotolewa katika sehemu ya chini ya waraka huu kwa maelezo zaidi.*

***Mwongozo huu haujanuiwa kuwa ushauri wa kisheria. Tafadhali kumbuka kwamba taarifa hii huenda ikabadilika katika muda wa wiki zijazo.*** **Mwongozo huu ulisasishwa mara ya mwisho mnamo tarehe 14 Aprili 2020**.

---

## Makazi

***Je, ninaweza kufurushwa kutoka kwa nyumba yangu ikiwa siwezi kulipa kodi?***

Pengine. Inategemea mahali unapoishi. Baadhi ya majimbo na miji imeharamisha tendo la mwenye nyumba kukufurusha wakati wa janga kubwa la COVID-19 au kwa kipindi fulani cha muda, hata ikiwa huwezi kulipa kodi yako.[1] Sheria ya ULINZI inaweka siku 120 za nafuu kwa baadhi ya ufurushaji kitaifa kwa wapangaji wanaoishi katika nyumba ambazo ni sehemu ya mipango ya serikali au walio na mikopo ya nyumba inayofadhiliwa na jimbo. Chunguza mtandaoni au na msimamizi wako wa kesi au shirika la msaada la mahali ulipo ili upate taarifa iliyosasishwa zaidi ya eneo lako. Huenda ukahitajika kutoa ushahidi ili kuonyesha kwamba kupoteza kwako mapato kumesababishwa na COVID-19. Iwapo unafurushwa, huenda ukataka kuwasiliana na Msaidizi wa Kisheria katika eneo lako. Tembelea https://www.lsc.gov/what-legal-aid/find-legal-aid kwa maelezo zaidi. Hata hivyo, kumbuka kwamba janga hili likiisha, huenda ukahitajika kulipa kodi za miezi ulizokosa kulipa na/au ada za kuchelewa.

## Ajira

***Je, ninaweza kuchukua muda wa mapumziko nikiwa mgonjwa? Iwapo ninahitaji kumlinda mtu ambaye ni mgonjwa au kuwalinda watoto wangu ambao wanakaa nyumbani?***

Pengine. Sheria za shirikisho, jimbo au za mtaani zinaweza kukuruhusu Uende likizo inayolipwa. Sheria mpya ya livu ya ugonjwa ya shirikisho huruhusu wafanyakazi katika biashara zilizo na idadi ya wafanyakazi chini ya 500 kuenda likizo inayolipwa ya ugonjwa ya siku 10 (au saa 80) kwa mshahara wako cha kawaida iwapo una dalili za COVID-19, uko kwenye karantini au unatafuta uchunguzi wa kimatibabu. Pia, unaweza kuchukua hadi wiki mbili (au saa 80) ya likizo inayolipwa ya ugonjwa kwa kiwango cha 66% ya mshahara wako wa kaida ili kulinda mtu ambaye ni mgonjwa au kulinda mtoto ambaye shule yake au mtoa huduma ya utunzi wa mtoto amefunga. Unaweza kuchukua wiki nyingine 10 za ziada za likizo inayolipwa ya familia na matibabu kwa 66% ya mshahara wako wa kawaida ili kuwatunza

---

[1] Kuhusiana na tarehe ya kuchapishwa kwa waraka huu, majimbo ya Arizona, California, Delaware, Hawaii, Illinois, Indiana, Iowa, Kansas, Kentucky, Louisiana, Maryland, Massachusetts, Michigan, New Hampshire, New Jersey, New York, North Carolina, Pennsylvania, Rhode Island, South Carolina, Tennessee, Virginia, Washington, wilaya ya Columbia na Wisconsin yote yana maagizo ya jimbo nzima yanayoharamisha kurufushwa kwa watu. Miji nyingi katika majimbo haya na mengine pia imerasimisha sheria sawa na hizi.

watoto ambao hawako shuleni au kituo cha kutwa cha watoto. Ni lazima uwe umeajiriwa kwa siku 30 ili upokee manufaa haya. Manufaa haya mapya ya ziada, hayapaswi kutumika kama mbadala ya manufaa uliyo nayo tayari hadi tarehe 31 Disemba 2020. Kumbuka, hata hivyo kwamba biashara zilizo na wafanyakazi chini ya 50 wanaweza kutaka kukataa likizo za kufungwa kwa shule na utunzi wa watoto iwapo kufanya hivyo kutahitilafiana na biashara.

Majimbo na miji nyingi pia ina sheria za likizo ya ugonjwa zinazowawezesha wafanyakazi kuchukua likizo iwapo ni wagonjwa au katika kisa cha janga la afya ya umma.  Angalia jimbo lako na eneo lako la utawala hapa: https://www.abetterbalance.org/covid19/

### *Je, ninaweza kufutwa kazi iwapo nitakuwa mgonjwa au kupatikana na COVID-19?*

Kulingana na Sheria ya Familia na Matibabu, mwajiri hawezi kukufuta kazi iwapo wewe ni mgonjwa. Ulinzi huu unapatikana kwa baadhi ya wafanyakazi pekee, hata hivyo, hasa wale ambao wamemfanyia kazi mwajiri fulani kwa angalau mwaka mmoja. Kwa maelezo zaidi, tafadhali zungumza na wakili wa sheria ya ajira.

### *Je, bima ya kukosa ajira ni nini? Je, nimehitimu kupokea manufaa ya kukosa ajira?*

Bima ya kukosa ajira ni manufaa ya pesa taslimu zinazolipwa kwa baadhi ya wafanyakazi waliopoteza kazi zao kupitia makosa ambayo si yao na kijumla wanapatikana na wanaweza kufanya kazi. Kila jimbo linatoa bima ya kukosa ajira kwa njia tofauti kidogo. Vilevile, Sheria ya ULINZI ya shirikisho (uwezeshaji) imepanua pakubwa uwezo wa kufikia bima ya kukosa ajira kwa kupungua au kuondoa mahitaji mengi ya jadi ambayo wafanyakazi walilazimika kufikia. Tazama majedwali haya ya ukweli na maswali yanayoulizwa mara kwa mara kwa maelezo zaidi: https://www.nelp.org/campaign/covid-19-unemployed-and-frontline-workers/.

Ili kutuma maombi ya manufaa ya kukosa ajira, tafuta jimbo lako kwenye tovuti hii: https://www.dol.gov/coronavirus/unemployment-insurance#find-state-unemployment-insurance-contacts.
Ili kuhitimu kupokea bima ya kukosa ajira, lazima uwe una uidhinishaji halali wa kazi wakati wa kipindi ulipokuwa unafanya kazi, na lazima uwe na uidhinishaji halali kwa kipindi ambacho unapokea manufaa. Hii inamaaniha kwamba wafanyakazi bila nyaraka hawawezi kupokea manufaa ya kukosa kazi. Unaweza kuhitaji kukagua miongozo ya jimbo lako ili uhakikishe kuhitimu kwako. Kukubali kupokea manufaa ya kukosa ajira **hakutamfanya** mtu kufungwa na kanuni ya "ada ya umma".

### *Je, ninahitaji kutoa ushahidi kwamba ninatafuta kazi huku nikipokea manufaa ya kukosa ajira wakati wa janga kubwa?*

Katika hali za kawaida, huenda ukahitajika kutoa ushahidi kwamba unatafuta kazi ili upokee manufaa fulani ya umma. Hata hivyo, wakati wa janga la virusi vya korona, huhitaji kutoa ushahidi wa "shughuli ya kazi" ili kufikia manufaa ya kukosa ajira. Baadhi ya majimbo bado yanakuhitaji kusajili vyeti vya kila wiki huku ukipokea manufaa ya kukosa ajira. Tafadhali pata kushauriwa kwamba sera hii huenda ikabadilika pindi tu janga hili likiisha.

### *Nikikatazwa kupokea manufaa ya manufaa je?*

Una siku 10 kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa shirika na lazima ufanye hivyo kwa maandishi. Pia huenda ukaweza kufikia Msaada wa Ajira wa Janga (PUA) badala yake, manufaa maalum kwa wafanyakazi fulani ambao kikawaida hawajashughulikiwa na bima ya kukosa ajira. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na ofisi yako ya bima ya kukosa ajira: https://www.dol.gov/coronavirus/unemployment-insurance#find-state-unemployment-insurance-contacts.

***Je, ninaweza kufutwa kazi au kubaguliwa nikimuuliza mwajiri wangu maswali kuhusu afya na usalama?***

La. ni kinyume na sheria kwa mwajiri wako kulipiza kisasi dhidi yako iwapo utaripoti hatari kwa usalama. Pia, hawawezi kukuhamisha, kukunyima kupanda kwa kipato, kupunguza saa zako za kazi au kukufuta kazi kutokana na afya yako. Una ulinzi zaidi wa kisheria iwapo unaweza kuandilkisha lawama unaohusiana na usalama na wafanyakazi wengine.

## Matibabu

***Ninaweza kujisajili kwa bima ya afya ya Medicaid wakati wa janga kubwa la COIVD-19?***

Unaweza kujisajili kwa tiba ya afya ya gharamaya chini hasa ikiwa hali yako ya ajira au mapato imebadilika. Hata hivyo, mchakato huo ni tofauti katika kila jimbo. Ukitembelea localhelp.healthcare.gov/#/, unaweza kuweka msimbo wako wa ZIP kisha uchague "Medicaid au CHIP" ili uone orodha ya watu katika eneo lako wanaoweza kukusaidia kujisajili. Unaweza pia kuzungumza na mtaalamu wa tiba ya kimsingi ikiwa unaye.

***Je, bado ninaweza kupata uwezo wa kumfikia mfasiri ninapompigia daktari wangu, polisi au huduma nyingine za dharura?***

Ndiyo. Bado una haki ya kupata huduma ya ufasiri, kama tu kabla ya janga. Hii inamaanishwa kwamba ikiwa unafikia huduma inayofadhiliwa na umma, kama vile mtoa huduma ya matibabu au polisi, una haki ya kupata huduma ya ufasiri na unapaswa kuuliza upewe mfasiri wa lugha uipendayo. Huenda ukapitia hali ya kusubiri kwa muda mrefu zaidi kutokana na kuongezeka kwa watu wanaohitaji huduma.

***Iwapo nitaenda hospitalini na nipimwe au nitibwe ugonjwa wa COVID-19, Je, hii itabadilisha halki yangu ya uhamiaji chini ya kanuni ya "ada ya umma"?***

La. Huenda ukawa na wasiwasi kuhusu kanuni ya "ada ya umma", mabadiliko ya hivi punde ya sera yanayoipa serikali uwezo wa kukataa hati ya makazi ya kudumu ya baadhi ya wahamiaji (green card) iwapo wamepokea manufaa fulani ya umma. Kanuni hii kwa ujumla hauwahusu wakimbili na waliokimbilia usalama kwa sababu wao ni vikundi vinavyolindwa vya wahamiaji chini ya sheria. Serikali pia imetangaza kwamba "huduma za matibabu na ulinzi zinazohusiana na COVID-19 hazitaathiri vibaya mgeni yeyote kama sehemu ya uchanganuzi wa Ada ya Umma siku zijazo." Hii inamaanisha kwamba kupimwa kwa au kupokea matibabu kwa COVID-19, hakutazingatiwa katika tathmini ya ada ya umma, hata ikiwa Medicaid au mpango mwingine wa serikali ukitumika kugharamia huduma hizo.

***Je, ninaweza kupimwa kwa ugonjwa wa COVID-19 ikiwa sina bima ya afya? Je, ni ghali?***

Serikali ilipitisha sheria mpya mnamo mwezi Machi ili kusaidia kulipia ada za kupima Virusi vya korona. Sheria hizi zitakusaidia kupimwa kwa virusi hivi bila malipo hata ikiwa huna bima ya afya. Ikiwa huna hati rasmi, uwezo wako wa kufikia huduma ya kupimwa bila malipo kunategemea jimbo unapoishi na kliniki zilizo katika eneo lako. Marekani kwa sasa ina upungufu wa vyombo vya kupima COVID-19, kwa hivyo kwa sasa huenda zisipatikane kwa kila mtu anayeviomba. Hata ikiwa kupima kunaweza kuwa bila malipo kwa ajili yako, tafadhali kumbuka kwamba *matibabu* ya COVID-19 si bila malipo na yanaweza kuwa ghali mno ikiwa huna bima. Iwapo una dalili za virusi vya korona kama vile, mafua kali na kikohozi kikavu, tumia Kikaguzi cha Kibinafsi cha Kituo cha Kudhibiti Magonjwa ili uone ikiwa wamependekeza utafute tiba katika https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/symptoms-testing/index.html.


*Waraka huu ulisasishwa mnamo tarehe 14 Aprili, 2020. Maelezo huenda hayajasasishwa.*

Ikiwa ni hivyo, unapaswa kumpigia daktari wako wa tiba ya kimsingi. Hakikisha umepiga 911 ikiwa unashuhudia dalili za dharura kama vile matatizo ya kupumua na maumivu ya kifua.

***Ninajihisi mpweke au mwenye wasiwasi. Ni nini kinaweza kunisaidia?***

Kujiweka mbali na watu kwa muda mrefu kunaweza kuwa jambo gumu. Hali isiyojulikana ya sasa inaweza kuwa ya msongo wa mawazo, kuchosha au kukulemea. Ukihisi kuwa mpweke sana au mwenye wasiwasi, tafadhali wasiliana na rafiki, jirani, jamaa au msimamizi wa kesi yako kupitia simu. Baadhi ya mikakati mingine ya kukabiliana na mfadhaiko au wasiwasi wakatri huu ni kukoma kusikiliza haditihi za habari au visasisho kwenye mitandao ya kijamii, kujaribu kutafuta muda kufanya shughuli unazozipenda, kula chakula chenye afya na kutembea ukihisi kuwa salama kufanya hivyo (huku ukidumisha umbali wa futi 6 au mita 2 kati yako na watu wengine).
Rasilmali zifuatazo pia zinaweza kusaidia:

- Tafakuri mtandaoni bila malipo (kwa Kiingereza): https://www.headspace.com/covid-19
- Rasilimali kutoka CDC, kitengo cha serkali kinachosaidia kupambana na magonjwa: https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/daily-life-coping/managing-stress-anxiety.html
- Mtu unayeweza kuzungumza naye iwapo uko kwenye janga (kwa Kiingereza): Piga simu nambari 1-800-985-5990, au tuma SMS yenye neno TalkWithUs kwa 66746

## Usalama

***Je, bado ninaweza kuripoti nikiwa mhasiriwa wa uhalifu? Je, vipi ikiwa sina hati rasmi?***

Ndiyo, bado unapswa kuripoti ikiwa wewe ni mhasiriwa wa uhalifu. Ikiwa unazungumza lugha nyingine na unahitaji mfasiri ili kuwasiliana, unapaswa kuomba huduma ya mfasiri. Afisa wa polisi anahitaji kutoa ufasiri wa kutosha. Taratibu za ICE za Utekelezaji na Uondoaji (ERO) zitaangazia utekelezaji kwa watu wale walio na rekodi za uhalifu na zitazingatia usiri ili kuchelewesha hatua za utekelezaji hadi baada ya janga au kutumia njia mbadala za uzuiaji, ilivyo muhimu. Hii inamaanisha kwamba hata ikiwa huna hati rasmi, bado unapaswa kuhisi kuwa salama kupigia polisi ikiwa unmekuwa mhasiriwa wa uhalifu. Baadhi ya wahasiriwa wa uhalifu pia wanaweza kuhitimu kupata manufaa ya uhamiaji, kwa hivyo baada ya kushirikiana na polisi, unapaswa pia kuwasiliana na wakili wa uhamiaji.

***Je, bado ninaweza kuripoti visa vya dhuluma za kinyumbani au dhuluma kwa watoto?***

Ndiyo, bila shaka. Ingawa mji au jimbo lako linaweza kuwa limewahimiza kila mtu kukaa nyumbani, wanafamilia wote bado wana haki ya kukaa katika mazingira salama na yaliyolindwa nyumbani. Unapaswa kupigia polisi ili kuripoti visa vya dhuluma au vurugu. Kwa kutegemea jimbo unapoishi, unaweza pia kuwa na uwezo wa kuandikisha Agizo la Kuzuia kwa Muda, kwa vile mahakama nyingi bado zimechukulia agizo hilo kuwa kipengele muhimu. Tafadhali pigia mahakama ya eneo ulipo kabla ya kujaribu kufika hapo.

Ikiwa unatafuta msaada au maelezo, unaweza pia kutraka kupigi National Domestic Violence Hotline kwa 1-800-799-7233. Simu niza siri na hazilipishwi, na mawakili katika nambari hiyo wanazungumza zaidi ya lugha 200. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yao: www.thehotline.org.

***Ninapaswa kufanya nini ikiwa mimi ndiye mhasiriwa wa uhalifu wa chuki?***

Kumekuwa na ongezeko la visa vya uhalifu wa chuki dhidi ya watu wenye asili ya Asia walio nchini Marekani. Ikiwa wewe ni mhasiriwa wa uhalifu wa chuki, unapaswa kuwasiliana na idara ya polisi katika eneo lako ili uripoti.

Wahasiriwa wa uhalifu pia wanaweza kuhitimu kupata manufaa ya uhamiaji na wanapaswa kuwasiliana na wakili wa uhamiaji baada ya kushirikiana na polisi.

***Je, ni lazima nitoe taarifa yangu binafsi kwenye simu ikiwa mtu ataniuliza kufanya hivyo?***

La, hupaswi kutoa taarifa binafsi au ya faragha kwenye simu au mtandaoni, kama vile nambari yako ya usalama wa kijamii au taarifa za benki. Kumekuwa na ongezeko la ulaghai wa simu na mtandaoni wakati wa janga la COVID-19. Ulaghai huu unahusisha watu wanaojaribu kuiba pesa zako, kutangaza tiba au matibabu ghushi ya COVID-19, kuahidi kukusaidia kufikia malipo ya kuwezesha watu kiuchumi au kujaribu kukuhadaa na ahadi za bidhaa ghushi wakati huu wa janga kubwa (kama vile simu za mkononi). Huu ni ulaghai na mara nyingi huwa kinyume na sheria. Watoa huduma halali hawawezi kukuuliza utoe nambari yako ya usalama wa kijamii au taarifa ya benki. Usihisi kushinikizwa kutoa taarifa kukuhusu, au hata anwani yako au tarehe ya kuzaliwa, isipokuwa ukiweza kuhakikisha kwamba ni mtu unayemwamini. Shirika la serikali haliwezi kukupigia simu kukuuliza utoe taarifa yako ya kibinafsi au kutishia kushikilia manufaa yako.

***Ikiwa jimbo au mji nilipo umewaarifu wakaazi "kubarizi mahali" au kuweka amri ya "kukaa nyumbani", je ninaweza kutiwa nguvuni kwa kutoka nje?***

Pengine. Baadhi ya maeneo yanawatia watu nguvuni kwa kukiuka amri ya "Kukaa nyumbani". Sasa hivi, hakuna amri inayotumika kote nchini, kila jimbo na/au mji inabuni kanuni zake. Kwa hivyo, inategemea hasa hali iliyopo katika eneo mahususi na maelezo ya amri. Kwa mfano, baadhi ya majimbo au miji imepiga marufuku mikutano ya hadhara ya zaidi ya watu 10. Baadhi ya majimbo na miji imepiga marufuku watu kuondoka nyumbani kwao isipokuwa iwe ni kwa orodha ya "shughuli muhimu," kama vile ununuzi wa chakula au kufanya kazi muhimu. Ni lazima uangalie vikwazo vilivyowekwa na jiji au jimbo lako mahususi. Tazama makala haya kwa maelezo zaidi:
https://www.cnn.com/2020/03/23/us/coronavirus-which-states-stay-at-home-order-trnd/index.html

## Uhamiaji

***Je ofisi za uhamiaji (USCIS) zinafunguliwa kwa sasa?***

USCIS (Huduma za Uraia wa Marekani na Uhamiaji) imesitisha huduma za ana kwa ana katika ofisi zote kote nchini. Kwa sasa wanapanga kufungua tena ofisi zako mnamo tarehe 4 May, lakini tarehe hii inaweza kuahirishwa tena kutegemea hali. USCIS itatuma taarifa ya kukatishwa kwa mahojiano na kuratibu upya watu wote waliotuma maombi watakapoanza tena kuendesha shughuli kikawaida.

***Je, nini inafanyikia ombi ambalo tayari nimewasilisha? Je, vipi ikiwa ninatafuta pa kukimbilia usalama?***

Vituo vyote vya huduma za USCIS bado vinafanya kazi kwa hivyo maombi ambayo yametumwa kwenye vituo vya huduma ambayo hayahitaji mahojiano, kama vile maombi ya kibali cha kufanya kazi na kesi za kuunganishwa tena kwa familia bado yanaweza kuamuliwa. Ikiwa una waraka wa kuidhinisha ajira au green card inayokaribia kukwisha muda, bado unaweza kutuma ombi la kuweka maombi hayo upya. Ikiwa ombi lako linahiaji mahojiano (ombi la kuunganishwa tena kwa familia katika balozi za kigeni au green card), basi mahojiano yako yataratibiwa (au kuratibiwa upya) pindi tu ofisi hizi zikifunguliwa tena. Ikiwa uko nchini Marekani kukimbilia usalama, bado lazima utume maombi ya kukimbilia usalama ndani ya mwaka wa kwanza wa kuwasili. Hakuna makataa mengine kando na haya wakati huu.


*Waraka huu ulisasishwa mnamo tarehe 14 Aprili, 2020. Maelezo huenda hayajasasishwa.*

***Je, ninahitaji kuhudhuria mahakama ya uhamiaji ili kusikiliza kesi yangu?***

Kesi zote za mahakama ya uhamiaji za watu ambao hawajazuiliwa zimeahirishwa hadi Tarehe 1 Mei 2020. Kuna uwezekano kwamba mahakama hizi za uhamiaji zitasogeza muda huu wa makataa. Ikiwa kesi yako imeratibiwa kusikilizwa wakati huo, itaratibiwa upya. Wakati wa kufungwa kwa mahakama kutokana na Virusi vya korona, nambari ya mahakama ya kiotomatiki ya 1-800-898-7180 huenda isisasishwe ili kuakisi tarehe yako mpya ya mahakama, lakini unapaswa kupiga simu ili uwe na uhakika. Unapaswa kupokea barua yenye taarifa ya tarehe mpya ya kusiklizwa kwa kesi. Unaweza kutembelea tovuti ya mahakama katika https://www.justice.gov/eoir/eoir-operational-status-during-coronavirus-pandemic ili uone ikiwa mahakama yako ya uhamiaji imefunguliwa au kufungwa karibu sana na tarehe ambapo kesi yako imeratibiwa kusikilizwa.

***Ninawezaje kupokea I-94?***

Iwapo ulipata kibali cha kukimbilia usalama kutoka kwa mahakama ya uhamiaji, kuna uwezekano kwamba hukupokea fomu ya I-94. Ni muhimu kupata fomu ya I-94 ili uwezu kutuma maombi kwa aina fulani ya manufaa. Iwapo ulipokea kibali cha kukimbilia usalama hivi majuzi na huna I-94, unaweza kutaka kupigia Kituo cha Mawasiliano cha USCIS kwa 1-800-375-5283. Ukiamua kupiga simu, maelezo ya I-94 kwenye ukurasa wa https://asyleeoutreach.org/common-questions/ yanaweza kuwa muhimu.

***Ikiwa nimeratibiwa kuingia kupitia mpango wa ICE. Ninapaswa kufanya nini?***

Inategemea mahali unapoishi; maafisa mbalimbali wa ICE wanatumia taratibu tofauti. Tunapendekeza kwamba uzungumze na wakili wako au uwasiliane na ofisi yako mtaani ikiwa kuingia huko kutfanywa kwa simu au kutaahirishwa.

## Malipo ya Athari za Kiuchumi/Kuwawezesha watu

***Je, nitapokea hundi kutokana na mpango wa kuwezesha watu kiuchumi?***

Serikali ilijumuisha kanuni katika Sheria ya ULINZI inayotoa malipo ya mara moja pekee ya kuwezesha watu kiuchumi ya hadi $1,200 kwa watu waliohitimu na hadi $2,400 kwa wanandoa waliohitimu. Familia zilizo na watu wanaowategemea walio chini ya umri wa miaka kumi na sita pia zinahitimu kupokea $500 kwa kila mtoto. Iwapo una maswali kuhusu kuhitimu kwako, unapaswa kzungumza na wakili wa ushuru au mwandaaji wa ushuru.

***Je, malipo ya athari ya kiuchumi inahesabika kama mapato kwa manufaa ya SNAP, TANF au SSI?***

La, malipo ya kuwezesha kiuchumi hayahesabiki kama mapato kwa muda wa miezi 12 na hayatozwi ushuru. Malipo ya kuwezesha kiuchumi ni ya kando na hayataonekana kwenye kadi yako ya manufaa.

## Mikopo ya Usafiri

***Je, ninaruhusiwa kuacha kulipa mkopo wangu wa IOM kwa muda ikiwa nitapoteza mapato yangu?***

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) huwapa wakimbizi mkopo wa usafiri ili kushughulikia gharama ya safari yao kuenda Marekani. Ka sababu ya mkurupuko wa COVID-19 na ugumu wa kiuchumi ambao watu wengi wanakabiliana nao, IOM inatoa urahisi fulani kwa wakimbikizi katika kulipa mikopo hii. Ikiwa huwezi kulipa mkopo wako, tafadhali

wasiliana na shirika linalosimamia mkopo wako li ueleze hali yako. Wanaweza kukusaidia. Ikiwa wewe ni mkimbizi au ulitafutiwa makao tena na HIAS, unaweza kuwasiliana nasi kwa 1-888-606-0565 au travelloans@hias.org.

## Kwa maelezo zaidi

*Tunatumai kuwa mwongozo huu umekusaidia. Iwapo una maswali yoyote kuhusu taarifa yaliyomo kwenye mwongozo huu au iwapo unatafuta rasilimali katika eneo lako, tafadhali wasiliana na msimamizi wa kesi yako au shirika la msaada la eneo ulipo. Unaweza pia kukagua rasilimali zilizo hapa chini:*

- Rasilimali hii ya mwongozo wa jozi ya lugha (Kiingereza/Kihispania) kwa ajili ya wahamiaji wasio na hati rasmi kutoka Immigrants Rising: https://tinyurl.com/t3vclo6
- Rasilimali hii ya mwongozo wa jozi ya lugha (Kiingereza/Kihispania) kwa ajili ya wahamiaji wasio na hati rasmi kutoka UndocuScholars: https://tinyurl.com/ss7munk
- Kwa maelezo ya kawaida, tembelea www.cdc.gov/COVID19
- Kwa maelezo kuhusu COVID-19 yaliyopangwa kulingana na lugha, tazama hapa https://tinyurl.com/uzhmuqf



*Waraka huu ulisasishwa mnamo tarehe 14 Aprili, 2020. Maelezo huenda hayajasasishwa.*